



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY – FOURTH SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 28th October 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:00 a.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

DEMISE OF KILIFI COUNTY ASSEMBLY SENIOR SERJEANT-AT-ARMS
MR. FELIX MWARABU

(The Speaker spoke off record)

The Speaker (Hon. Kahindi): ...Hon. Members, because of this, I hereby suspend all the business that the County Assembly had intended to transact today and instead take this moment to give Members of the County assembly an opportunity to eulogize Mr. Felix Mwarabu who until the time of his death served the County Assembly as the Senior Serjeant-at-Arms. It was only last week when we walked with him in this Chamber during the procession. We loved him but God loved him more.

Hon. Members, I know it is a very emotional moment for us. We will understand if you may not be able to hold yourself together but let us take this time to reflect on his memories and then have the House adjourned until after the recess. Thank you.

Hon. Shaban: Thank you Mr. Speaker, Sir. It is hard to believe that the Senior Serjeant has left us. As we mourn his demise, I wish to also say that if the House can also get to know

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

exactly what happened maybe from the time Mr. Mwarabu was sick, the first hospital he visited and how he was received at the Kilifi County Hospital.

I want to also pass my sincere condolences to the family of Mr. Mwarabu and the family of the County Assembly of Kilifi. We have lost a person who was always there for us. He was humble. I made a habit that every time I came to this House I would pass by his office and every time I would go there we would talk in a good way before I proceed to this House. This House will remember Mr. Mwarabu for many years to come. May his soul rest in peace. Thank you.

Hon. Mwambire: Asante sana Bw. Spika kwa nafasi hii. Nimesimama pia nipeane rambi rambi zangu kwa jamaa na marafiki wa ndugu ambaye tumekuwa pamoja hapa na ametuacha kwa njia ya kuhuzunisha. Tulikuwa na yeye hapa Jumatano iliyopita na hatukuwa tunajua ni mgonjwa na hatukuwa na matazamio ya kwamba yale yaliyomfika yangemfika. Nimemfahamu Felix Mwarabu kabla ya kukutana hapa na ni mtu ambaye alikuwa anaishi kwa undugu na unyenyekevu wa hali ya ajabu sana. Mbali na hivyo, katika uadilifu wa kazi pia alikuwa nao.

Sitakuwa na mengi ya kuzungumza ila tu kuiombea roho yake marehemu Felix Mwarabu Mungu akaweze kuirehemu. Amsamehe alipoenda kinyume na mapenzi yake. Aiweke roho yake mahali pema. Vile vile jamii iliyoachwa Mungu awape nguvu na sisi sote kwa ujumla kama Bunge atupe nguvu ya kustahimili jambo hili. Asante mheshimiwa Spika.

Hon. Mbura: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Nina mengi ya kunena lakini kwa sasa nataka nichukue mda mfupi ili kutoa neno langu la pole kwa familia ya ndugu yetu, aliyekuwa *Serjeant* wetu Felix Mwarabu. Mimi binafsi, Felix Mwarabu, nimemjua maisha yangu yote. Tumesoma shule moja. Nikiingia kidato cha kwanza yeye alikuwa anatoka kidato cha nne. Nina uchungu sana haswa niliposikia kifo chake cha ghafla. Kusema kweli, ni hali ngumu sana kwetu sote hapa na pia wafanyikazi wa Bunge hili na vile vile Kaunti nzima kwa sababu Felix alikuwa ni mtu wa watu. Alikuwa na utu na kupenda watu. Langu ni kusema tuweni pole sote na tuzidi kumshukuru Mungu kwa haya aliyotutendea kwa ndugu yetu na tuzidi kudumisha upendo kati yetu hata baada ya haya yote ambayo tumepitia.

Tuzidi kuombea familia na inapowezekana pia sisi kama waheshimiwa na Bunge nzima tukumbuke familia yake aliyoiacha. Yuko na watoto wanasoma, ni watatu; mmoja yuko Bahari Girls, mwengine yuko Godoma Technical na kuna mdogo pia anahitaji kulelewa. Tuweze kukumbuka familia baada ya kumsindikiza ndugu yetu Felix. Asante kwa nafasi hii. Wacha Mungu amlaze mahali pema alipomchagulia. Asanteni.

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker, for granting me this opportunity. First of all, I want to give my heartfelt and sincere condolences to the family of the bereaved; our late brother Senior Serjeant Felix Mwarabu. It is with sorrow that I learnt the death of our brother and as of yesterday, I was trying to find out the real cause of his death.

As a Christian, I believe our lives lie in the hands of God but at the same time we need to be careful because there is something which human beings contribute. Yesterday I tried to check on the movements of our brother before he passed on and I got information that he was attended to here in Malindi. I do not want to mention the hospital he was attended at then referred to Kilifi in a vehicle that did not have oxygen. When he got to Kilifi, there was some kind of negligence at the hospital. I felt very bad when I got this information.

In my view, can we form a committee that will find out what really happened so that we get the correct information? I am saying this because of the kind of negligence that we have in our hospitals; someone is just left there for more than half an hour with no one attending to him. The attendants in the hospitals should be concerned especially in this time of the pandemic. The

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Committee on Health can also try to get more information so that we can rectify the situation because today it's him tomorrow it is me and you.

Hon. Kenga: Shukrani sana mheshimiwa Spika kwa nafasi hii niseme machache kuhusu kifo cha mmoja wa wafanyikazi wetu ambaye ametuacha. Nina uchungu sana uliponipigia siku ya Jumapili kuniuliza kama nimepata habari. Nilipigwa na mshangao mkubwa kwa sababu nilikuwa sijazipata. Kifo chake kilinishangaza kwa sababu ndani ya ile wiki alipofikia mauti tulikuwa naye katika kazi, hata kwa sasa bado tuko katika mshangao. Huyu ni miongoni mwa wafanyikazi waliowajibika katika kutekeleza majukumu yao. Alikuwa na mchango mkubwa sana ya vile sisi kama waheshimiwa tunaendesha shughuli zetu hapa Bungeni na hata kule nje katika shughuli za Kamati. Sio kwa urefu wa mtu kuishi katika ulimwengu *but what matters is how well one lives in this world*. Kwa ule muda mfupi tuliomjulia Mwarabu tofauti na mheshimiwa Kazungu waliojuana tangu shule, tumeshirikiana vizuri kwa kazi na shughuli nyingine.

Nilipofanya harusi yangu tarehe moja mwezi wa nane mwaka wa 2015, kuna mengi tulioshirikiana. Wakati huu niko na uchungu mwingi kwa sababu ya pigo hili. Tukiwa katika hali ya majonzi tujue nini hasa kilichangia kifo chake. Kama vile waheshimiwa wametangulia kusema kwamba kuna hali ya watu kuzembea kwa kazi. Sasa ninaomba uchunguzi ufanywe ili tuwe na uhakika nini kilifanyika na iendapo kuna mtu alilegea kazini tuko na nafasi ya kurekebisha ili kuepusha mambo kama haya. Pia naomba kama kuna kitu tunaweza kufanya kama serikali ili ibaki kama kumbukumbu jinsi alivyojitolea kufanya kazi ili isiwe baada ya maombolezi historia yake isahaulike, kama ni barabara, shule ama sehemu yoyote ya umma inayoweza kutambulika katika jina lake ili tumkumbuke kwa mema aliyofanya. Kwa hayo, wacha niseme pole kwa familia na wote waliojuana naye na Mungu atufaraji.

Hon. (Ms.) Elina: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii nichangie kuhusu mfanyikazi wetu Bw. Mwarabu. Mwarabu mwaka wa 2013 alijiunga na Bunge la Kilifi na tangu tuwe naye nakumbuka jambo jema alilolifanya siku moja tulipokuwa tumeenda kwa *Devolution* kule Kisumu. Kulikuwa na baadhi ya waheshimiwa wengine wamelewa kiasi cha kuwa wamekosa fahamu mahali Fulani. Mwarabu alimkimbiza yule mheshimiwa na kuenda kumuweka mahali pazuri ili wengine wasijue na wengine hawakujua. Roho ya Mwarabu haifananishwi na mtu mwengine hapa.

Tuko na wafanyikazi Bunge hili; kuna wengine wamejitokeza na kupenda kazi yao na kuifanya vyema, wa kwanza akiwa ni Mwarabu. Tangu aingie Bunge hili hajakuwa na mgogoro pengine mheshimiwa ameingia Bungeni bila kuvaa nadhifu, angemuambia mheshimiwa nenda ubadilishe kitu fulani kwa ofisi yangu urudi hapa ukae vizuri. Hakuna siku aligongana na mtu hata siku moja. Wema ule alioufanya Mwarabu kwa Mungu alikuwa na thawabu na kizuri Mungu pia anakipenda.

Tukumbuke sisi sote ni mali ya Mungu na wakati wowote Mungu atakuita. Jambo liliolozungumzwa na mheshimiwa Peter Ziro; nakumbuka 2013 mheshimiwa Spika ikiwa wewe ndiye Spika wa Bunge hili kuna siku moja nilianguka na *pressure* na nikalazwa pale hospitali ya Tawfiq. Kabla sijatoka kwa boma langu nilijaribu kushika simu kumpigia Amos. Amos akakimbiza gari na kuja kunipeleka kituo cha hospitali na nikahudumiwa vizuri sana. Nilipotoka pale nilisema kama ni familia yangu ingelishindwa lakini Bunge lilinisaidia. *Communication* hiyo ningeliomba katika Bunge hili kama pengine mtu ameanguka mahali lakini ana nafasi ya kupiga simu katika Bunge asaidike kwa haraka na aponeshe roho yake nafikiri mheshimiwa Spika utupe hiyo ruhusa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kilichotendeka kulingana na historia kwamba alienda walipofika karibu na Kilifi akasema anahisi baridi akasema gari isimamishwe na aliposimamishwa pale kando ni kama Felix alikuwa ameaga. Walipofika pale hospitali ilikuwa ni kama alikuwa amemalizika. Kifo hiki kimeturegesha nyuma tena kama wakati wa mheshimiwa Chihanga alipoaga, na leo ni *staff*. Maoni yangu nasema hata kikao hiki kikiendelea wengi itakuwa ni kama tunahuzunika maana tunakumbuka alivyokuwa akitembea katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naiombea ile familia maana imepoteza mtu wa maana aliyekuwa akijali wenzake... Kuna wengine hawajali watu hapa na tunawajua lakini kwa nini kila mtu analia kwa ajili ya Mwarabu. Ni heshima yake na taadhima aliyokuwa akiifanya hapa Bungeni hakika hatutasahau. Alikuwa anajitolea yeye mwenyewe. Wakati tukimzika Chihanga alitoka na mwili kutoka Mombasa na tukaenda sote mpaka Kambe, tukalala asubuhi yake tukashinda ndio tukamzika mheshimiwa Chihanga. Nitakumbuka kifo hiki kilichomchukua ndugu yetu Felix Mwarabu lakini pia tusilaumu sana maana Biblia inasema siku za kuishi mwanadmu si nyingi kisha zimejaa taabu; zile taabu amekumbana nazo ndugu yetu wacha Mungu amlaze maana mwendo ameumaliza. Tunachoomba ni wale watoto wake Mwenyezi Mungu awape neema, awape faraja ya ajabu na Bunge hili wingu la faraja litande juu yetu tuweze kumzika ndugu yetu Felix na aagane nasi tuingoja siku zetu zilizobakia katika ulimwengu huu. Nasema asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii.

Hon. Mkadi: Asante mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Nami pia nitoe rambi rambi zangu kwa familia, sisi pia hapa Bunge na wale wenzake ambao alikuwa anafanya nao kazi kitengo kimoja kwamba Mwenyezi Mungu ametupa na Mwenyezi Mungu amechukua. Nasema kazi yake haina makosa. Ni kweli kwamba mtu akifariki huwa anapewa sifa za kila aina. Mimi binafsi Felix sikunjua mda mrefu; nilimjua baada ya kujiunga na Bunge hili lakini kiukweli, alikuwa akifanya kazi yake vizuri kwa sababu kama mimi mgeni kuna ambayo labda kwa mda fulani yatakuwa labda siyaelewi. Alikuwa ni mtu ambaye anaweza kukuita na akakupatia ushauri wa njia ambayo inatajikana uifuata. Sasa ni pengo ambalo limekumba Bunge hili. Tunasikitika kwamba familia imeachwa na mtu wa karibu lakini hata sisi pia hapa tumeachwa na mtu ambaye ilikuwa tukimtegemea kwa njia moja ama nyengine. La msingi ni kumuombea kule anakoenda na amueke alipojichagulia. Zaidi ya yote aipe familia matumaini maanake maisha lazima yaendelee sisi tukiwa kama watu ambao tulikuwa karibu naye, tujaribu tuone ni vipi tutasaidia familia ili mbali na kuwa tumesema pole lakini tuelekeze kwamba ile familia haitahuzunika kwa kujaribu kuziba lile pengo ambalo ndugu yetu ameliacha.

Pia kwa sababu kifo hatuagani nacho kila mtu anatembea hapa na huenda ikawa sisi pia ni marehemu watarajiwa, kesho ama siku nyengine. Basi tuweke mioyo yetu vizuri; tuamini kwamba kila aliyeletwa hapa duniani ipo siku ataondoka. Tujitayarisha ili siku zetu zinapofika tujue tutapokelewa vipi kule mbinguni. Asante mheshimiwa Spika kwa hiyo nafasi.

Hon. (Ms.) Radhia: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii kwa kusimama na kuweza kumuombea mwenzetu Felix Mwarabu ambaye ametuacha juzi. Kwanza kabisa, ningependa kumuombea kwa sababu chakula cha maiti ni dua. Kwa hivyo, ningependa muinue mikono na tuweze kumuombea. Mtaitikia *Amin*. Hii ndio duwa ambayo sisi Waislamu humuombea maiti.

(Hon. (Ms.) Radhia said a short Islamic prayer)

Mheshimiwa Spika, hili Bunge kama unavyoliona lina huzuni kubwa na kila mmoja ana masikitiko kwa Felix. Felix ana sifa za kipekee. Mimi nikinakili Felix alikuwa hana ubaguzi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Alipokuwa akifanya kazi katika Bunge hili hakuwa na ubaguzi wa dini, hakuwa na ubaguzi wa rangi, hakuna na mkubwa wala mdogo. Yeye alifanya kazi kama alivyotakiwa kufanya kazi. Sote hapa leo kama mama *Ngangari* alivyosema tunasikikitika kwa sababu alitimiza wajibu wake kwa kila mtu.

Ukienda kwake na matatizo yako yule alikuwa anatafuta njia ya kutatua. Tunaomba yule atakayechukua nafasi hii awe kama Felix Mwarabu. Sitakuwa na mengi maana huzuni ndio nyingi zaidi. Kama nilivyosema katika *forum* ya MCA 003, tumepoteza mtu wa maana sana na sidhani kama kuna mtu atakayekuwa kama yeye. Alitulinda na tukampenda lakini Mwenyezi Mungu alimpenda ziadi. Chakula cha maiti sio machozi.

Hon. Reuben: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa hii nafasi ya kutoa rambi rambi zangu kwa niaba ya mfanyakazi mwendazake Felix Mwarabu. Kwa uhakika sijamjua kwa kipindi kirefu maana niliingia hili Bunge mwaka jana mwezi wa kumi. Katika mda mchache ambao nimekuwa hapa, nimeona maneno ambayo Mwarabu alikuwa akifanya yakugusa moyo. Mwarabu alikuwa anapeana mkono wa urafiki kwa yule aliyemjua kitambo na aliyemjua juzi juzi; wote anawachukulia kisawa. Ni juzi tulikuwa naye tukizunguka na Kamati ya Ardhi kuhusu mpangilio ya miji, tukaitwa na *Executive* na tulikuwa tunawadai zaidi ya shilingi 100,000. Tukaongea maneno pale akasema nina mambo yangu nataka kuyafanya Mungu akinijalia nikipata hizi pesa nitamaliza mambo yangu lakini Mungu alikuwa amepanga.

Mwarabu ameenda lakini mimi hukumbuka maneno na ukimiruhusu nitayasema kwa njia ya nyimbo...

(Hon. Reuben sang a gospel farewell song)

Mambo kama haya yanapojiri hunikumbusha mambo ya ndani. Mwarabu kazi yake hapa duniani imeisha na amevaa kutoharibika; ni matendo yake ndio yanayoongea sasa. Kuna msemu unaosema, “*what matters in life is not how wealthy you are but how many people smile or laugh because of you.*” Machozi yanayoonekana katika mioyo ya waheshimiwa na wafanyakazi hapa ni kwa sababu ya matendo ya Mwarabu yaliyofanya wengi wacheke. Mungu ailaze roho ya Mwarabu pahali pema peponi.

Hon. (Ms.) Winfred: Asante Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Nikichangia tu kidogo nimesimama kwa niaba ya Kamati ya Ardhi. Mwarabu alikuwa mlinzi wa Kamati. Tumekuwa tukizunguka Kaunti ya Kilifi kwa ajili ya mipangilio ya miji. Ilifikia mahali Mwenyekiti alikuwa hayuko nilikuwa nashikilia mkutano; alikuwa anahakikisha saa kumi na mbili amenipigia simu kuniambia usichelewe kwa ajili ya kuanzisha mkutano, na nikifika pale alikuwa anasema mheshimiwa kama umepewa majukumu usichelewe fanya kazi kwa ustadi, na alihakikisha kila mahali tukienda tuko salama.

Nakumbuka tulipokuwa na mkutano kule Kakuyuni kulipokuwa na mvutano na vita, Mweyekiti alisimama na akasema hii Kamati haitembei peke yake inatembea na polisi na Mwarabu alisimama na kukawa shwari. Ninashukuru kwa muda nimekuwa na Mwarabu hapa. Kazi ni kwa muda mchache lakini kule nyumbani yeye ni wa karibu sana. Nilipoingia hapa alikuwa kama mshauri wangu. Aliniambia mheshimiwa umefika Bunge nataka ufanye kazi usiniabishie kule Chonyi. Lingine Mwarabu hakuwa na ubaguzi. Wacha ikumbukwe kwamba yeye alikuwa mchapa kazi na pia ako na mchango mkubwa kwa ajili ya maendeleo kwa makundi ya watu huko nje. Tunafaa kukumbuka kwamba hapa duniani sisi ni wasafiri na hujui hata dakika chache zijazo utakuwa wapi. Tujipange ili wakati wetu unapofika tukatoke tukiwa tumejitengeneza hapa duniani. Ni hapo. Asante mheshimiwa Spika.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Chengo: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatika nafasi ili nami kunena machache kwa ajili ya mpendwa wetu Felix. Kwa huu mda mchache ambao nimemjua Felix, nimemuona ni mtu wa maana sana; hana ubaguzi wala kuona huyu labda ametoka wapi. Kila atakayemuona alikuwa ni ndugu ama dadake na anahusiana na kila mmoja. Kwa hakika Bunge hili tumepoteza mtu wa maana na kwa sababu ilikuwa ni wakati wa Mungu kwamba aende kama labda mtu angeulizwa nani angeenda hatungewahi kusema Felix lakini kwa sababu ni mpango wa Mungu, nasema kwamba Mungu aweze kutufaraji sisi sote kwa sababu amechukua mtu ambaye kwetu alikuwa ni wa maana sana lakini kwa sababu ameenda, atufaraji ili tuweze kuingiliana na ile hali jinsi ilivyo.

Sitakuwa na mengi sana. Naomba tu Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Tukutane tena nasi tukienda huko. Mungu awabariki sana.

Hon. (Ms.) Messo: Asante sana Bw. Spika. Nimesimama hapa kama mheshimiwa Philister (Messo). Habari ya Felix siwezi kuongea sana lakini naomba Mwenyezi Mungu aweke roho yake mahali pema peponi. Asante.

Hon. (Ms.) Victoria: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa rambi rambi zangu pamoja na familia yangu. Mimi sikumjua Felix kwa mda mrefu. Nilimjua tu nilipoingia katika hili Bunge lakini baadaye nikaja kugundua kwamba ni *family friend*. Amesoma na baadhi ya mashemegi zangu. Kwa hivyo nikaja kujua kwamba ni mtu ambaye alitambua sana familia yangu tangu kitambo ilikuwa ni familia ambazo zinajuana. Alisoma Jaribuni *Secondary* na alikuwa akienda shule mpaka apitie pale nyumbani. Kwetu ni katikati ya Jaribuni *Secondary* na kwao kwa hivyo alikuwa mpaka apitie pale ashikane na wale rafiki zake ndio waende shule.

Tangu niingie hili Bunge, Felix alikuwa na moyo ambao hata mimi naweza sema siuwezi kwa sababu kuna siku hata nilimuuliza swali; nilimuuliza, “kisha wewe hukasirika?” Akacheka. Yeye alikuwa wa kupenda kucheka. Akaniuliza, “kwa nini mheshimiwa?” Nikamwambia, “sijawahi kukuona umekasirika hata siku moja.” Akasema, “huwa nakasirika lakini kimoyomoyo.” Sijawahi kumuona amekasirika ama kushikwa na hasira na pengine kusema maneno ya kuudhika. Alikuwa mtu wa furaha sana.

Ungekuwa na matatizo, Felix angekutafuta yeye aje akuambie wewe unajua kuna jambo fulani ama kuna karatasi fulani unatakiwa ujaze wakati mwenyewe huna hata habari. Yeye ingesumbua mpaka akutafute uje ujaze ili pengine ni kitu ama malipo yangekupita na pengine hukujua kuna karatasi inatakikana ijazwe angekuambia basi kuna hizi karatasi wenzako wamejaza pengine wewe hujajaza. Nakumbuka alinisaidia wakati nilikuwa nimechukua *loan* na pesa hazikuwa inakatwa kwa *payslip*; akasema nenda kwa HR ukashughulikia hili jambo ili wakati unatoka lisikuletee shida. Sisi ambao tumebaki tuige mfano wake. Aliishi ni kama alijua hakuwa na siku nyingi za kuishi; alikuwa anabeba mzigo ya wenzake kama yake na alikuwa ni mtu ambaye kama ana jambo lolote ambalo litakusaidia atakuambia.

Nilipigiwa simu na mheshimiwa Riziki aliponielezea kwamba Mwarabu amekufa; sahani niliyokuwa nimeshika sijui ilianguka vipi. Ilibidi nimpigie Omar akasema ni kweli hata saa hii tuko hospitali; niliona dunia imegeuka rangi. Kifo kiko hata kwa *group* ya waheshimiwa niliandika *death is real*. Mwarabu alikuwa na ukaribu na sisi. Hata leo nimekuja nikaona ile picha yake nikaona labda watu wanafanya sarakasi; nimeenda mpaka ofisini nikifikiri nitamuona atoke tusalimiane. Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. Sina la kusema kwani nimepoteza rafiki na msaidizi. Mungu anajua yote. Mwarabu ameniliza tangu kifo chake mpaka saa hii sijaamini mimi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ADJOURNMENT

SHORT RECESS

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, I wish to adjourn this House for the Short Recess that is starting today, ending on the 8th of November. Further communication in regards to the burial arrangements will be communicated through the Office of the Clerk. Thank you very much.

The House rose at 10:55 a.m.